

HALMASHAURI YA WILAYA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

WILAYA YA KONDOA
Fax/Simu 026 2360313
E-Mail: ded@kondoadc.go.tz



Sanduku la Posta 1
KONDOA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya KondoA anatangaza nafasi za kazi. Maombi ya kujaza nafasi yoyote kati ya hizo yanakaribishwa kutoka kwa Mtanzania yeyote mwenye sifa zilizotajwa katika tangazo hili.

Nafasi zinazotangazwa ni kama ifuatavyo:-

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II: Nafasi 1

Majukumu:

- (i) Kutafuta kumbukumbu/majalada yanayohitajiwa na wasomaji
- (ii) Kuweka majalada katika makundi
- (iii) Kuweka kumbukumbu(barua,nyaraka, n.k)katika majalada
- (iv) Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/ nyaraka.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:-

- (i) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Sita (VI)
- (ii) Awe amehitimu mafunzo ya Utunzaji wa kumbukumbu angalau katika ngazi ya Cheti katika mojawapo ya fani za Afya,Masjala, Mahakama au Ardhi.

2. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III: Nafasi 05

Majukumu:

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- (ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao,kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.

- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- (v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
- (vi) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji

Mwombaji awe na Sifa zifuatazo:-


- (i) Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV)/Sita (VI)
- (ii) Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

Vigezo na Masharti ya Jumla kwa waombaji:

- (i) Mwombaji awe raia wa Tanzania
- (ii) Awe na umri na usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18
- (iii) Maombi yote yanaambatanishwe na nakala ya cheti cha Taaluma, Nakala ya Cheti cha kidato cha nne/sita, maelezo binafsi(CV), picha(passport size mbili) za hivi karibuni.
- (iv) Vyeti vyote vya Taaluma na kidato cha nne/sita ni lazima vithibitishwe na Hakimu au wakili anayetambulika na Serikali.
- (v) Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu, maombi yake hayatashughulikiwa.
- (vi) Watumishi ambao walikwisha ajiriwa hapo awali na kupangiwa vituo vya kazi katika maeneo mengine hawaruhusiwi kuomba.

Barua zote zitumwe kwa njia ya Posta, maombi yatakayowasilishwa kwa mkono au barua pepe hayatafanyiwa kazi.

Tangazo hii limetolewa tarehe 28/08/2017 na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/09/2017 saa Tisa na nusu Alasiri.


Mwl. Falesy Mohamed Kibassa,
MKURUGENZI MTENDAJI (W),

KONDOA

**MKURUGENZI MTENDAJI
KONDOA**

TILAZA